

**HOTUBA YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. KASSIM M. MAJALIWA (MB) WAKATI AKISHUHUDIA ZOEZI LA UCHEPUSHAJI WA MAJI YA MTO RUFJI ILI KUPISHA UJENZI WA TUTA KUU LA BWAWA LA JULIUS NYERERE TAREHE 18 NOVEMBA, 2020**

Mhandisi Zena Said, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati;

Dkt. Alexander Kyaruzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati;

Dkt. Asim Abdelhamid Elgazar, Waziri wa Nyumba;

Dkt . Mohamed Elmarkabi, Waziri wa Nishati wa Misri;

Dkt. Medard Kalemani, Waziri Mstaafu wa Nishati;

Dkt. Hamdy Loza, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri;

Makatibu Wakuu, Naibu Katibu Wakuu na Viongozi wengine wa Serikali;

-Dkt Damas Ndumbaro, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (Utawala Bora);

-Prof Sifuni Mchome, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria;

-Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu - IKULU;

-Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje;

-Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;

-Naibu Makatibu Wakuu mliopo;

Dkt. Alexander Kyaruzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO;

Balozzi Mohamed Elwafa, Misri nchini Tanzania;

Bw. Mohamed Abdelwahab, M/kiti Bodi ya Uwekezaji ya Arab Contractors (Misri);

Bw. Sayed Elbaroudy, Mwenyekiti Bodi ya Arab Contractors (Misri);

Bw. Sadek Elsewedy, Mwenyekiti Kampuni ya Elsewedy Electric (Misri);

Bw. Hesham Okasha, Mwenyekiti Bodi ya Benki ya Ahly (Misri);

Jen. Kamal Barany, Msaidizi wa Mkuu wa Kikosi cha Uhandisi katika Mamlaka ya Jeshi (Misri)

Dkt. Tito Mwinuka, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO;

Mha. Kashubila, Mhandisi Mkazi wa Mradi;  
Wafanyakazi wa TANESCO, TECU na Wakandarasi;  
Viongozi wa Serikali kutoka Taasisi mbalimbali;  
Waandishi wa Habari;  
Wasanii Wetu;  
Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;

## **UTANGULIZI**

Awali ya yote nitangulie kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha wote kukutana hapa siku hii ya leo katika hafla hii fupi ya kushuhudia uchepushwaji wa maji kutoka Mto Rufiji,

Leo nimekuja na salaam kutoka kwa Mhe Dkt John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati na za kipekee kwa ushirikiano mkubwa unaotolewa na Serikali ya Misri katika kuhakikisha Mradi huu wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere unakamilika kwa wakati.

Ndugu Watanzania mtakumbuka wakati wa kampeni, viongozi wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ilani ya CCM waliahidi kuendeleza miradi yote iliyoanzishwa. Shukrani kwa kumpigia kura nyingi Dkt John Pombe Magufuli na hii ni ishara ya imani ya kazi zilizofanywa ukiwemo mradi huu.

## **GHARAMA NA MANUFAA YA MRADI**

Mradi huu unafadhiliwa na Serikali kwa asilimia 100, kwa gharama ya **Shilingi trilioni 6.557**. Aidha, Serikali imeendelea kuwaamini na kuwatumia Wataalamu wa kitanzania katika kusimamia miradi mikubwa na kwa kutambua hilo mradi huu unasimamiwa na Mhandisi Mshauri wa kitanzania kwa asilimia mia moja.

**Mabibi na Mabwana**, mradi huu wa Kufua Umeme kwa kutumia maji wa Julius Nyerere ni mradi mkubwa, wa kimkakati na wa aina yake katika ukanda huu wa Afrika, ukiwa ni wa kwanza kwa ukubwa kwa Afrika Mashariki na wa nne katika Bara la Afrika.

Nimeambiwa kwamba, Mradi huu unaenda sambamba na ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya msongo wa kilovolti 400 kutoka eneo la Mradi hadi Chalize, yote hii ni kuhakikisha umeme unaotoka hapa unaingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Niipongeze Wizara yetu ya Nishati, TANESCO, Wakandarasi na TECU kwa juhudi kubwa mnazoendelea nazo kutekeleza mradi huu mkubwa wa Julius Nyerere pamoja na ubunifu wa miradi mbalimbali ya nishati na umeme.

**Ndugu Wageni Waalikwa**, kama mnavyofahamu Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Nchi inakuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika. Kwa kutambua hilo tumeweka vipaumbele katika Sekta ya Nishati nchini. Serikali imehakikisha hali ya upatikanaji wa umeme inaimarika na huduma za kijamii na kimaendeleo zinawafikia wananchi. Lengo kubwa likiwa ni kuboresha hali ya maisha ya Watanzania wote kwa ujumla pamoja na kuchochea fursa za kimaendeleo na kiuchumi kwa wananchi wote.

**Ndugu Wageni waalikwa**, upatikanaji wa umeme wa bei nafuu na uhakika nchini kwetu utachochea ukuaji na mapinduzi katika sekta ya viwanda kwa kushusha gharama za uendeshaji viwandani, kukabiliana na mfumuko wa bei, kuwezesha ushindani wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya Afrika Mashariki, Afrika na Duniani kwa ujumla sambamba na kuvutia uwekezaji mkubwa wa kati na mdogo katika sekta mbalimbali nchini kutokana kupungua kwa gharama za umeme katika uzalishaji pamoja na watanzania wote kumudu gharama za umeme mijini mpaka vijijini.

Aidha, mradi huu utatuwezesha kuwa na umeme mwingi, na wa kutosha lakini pia kutuwezesha kufanya biashara ya umeme na nchi jirani.

**Ndugu Wageni waalikwa**, kuimarika na kukua kwa sekta ya Viwanda kutokana na Mradi huu, Shirika letu la Umeme, TANESCO litanufaika kwa kuongeza makusanyo ya bili za umeme za kila mwezi kutoka kwa wateja wakubwa na viwanda vitakavyojitanua na vipya vitakavyounganishwa.

Mapinduzi hayo yote yanatarajiwa kuzalisha ajira nyingi kwa kiasi kikubwa, kuongeza mapato ya kodi kwa Serikali na hivyo kukuza pato la mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla pamoja na kuimarisha uchumi wa Nchi. Maendeleo hayo na upatikanaji umeme wa uhakika utakwenda sambamba na kuimarika kwa huduma za kijamii kama vile maji, elimu, afya, teknolojia, n.k.

**Ndugu Wageni waalikwa**, umeme ni huduma muhimu ambayo ikipatikana na kutumika vizuri inaweza kuondoa kabisa umasikini katika nchi yetu kwa ujumla.

## **HATUA ILIYOFIKIWA**

Kwa kutambua umuhimu wa mradi, Mhe. Dkt John Pombe Magufulu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua kutekeleza mradi huu wa umeme wa Julius Nyerere ambayo ilikuwa ni ndoto na maono ya Baba wa Taifa letu, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere ambapo leo hii mradi huu umefikia hatua muhimu ya kuchepusha mto kwa ajili ya kuanza rasmi ujenzi wa tuta kuu la kingo za bwawa litakalotumika kuzalisha umeme huo. Niyapongeze makampuni yanayojenga mradi huu ambayo ni *Elsewedy Electric* na *Arab Contractors* kwa kazi nzuri na ahadi ya kumaliza kwa wakati.

## **MAAGIZO MUHIMU**

**Ndugu Wageni waalikwa,** kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza nasisitiza usimamizi makini, wa viwango na madhubuti kwa mkandarasi kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika kwa wakati kama ambavyo sisi tunalipa kwa wakati. Pili kutekeleza makubaliano ya CSR ili tuanze kutekeleza miradi tuliyojipangia.

Pia nitumie nafasi hii kuwahimiza wataalamu wetu wa ndani kutumia fursa hii ya kujengewa uwezo kwa manufaa ya baadae katika kusimamia mradi huu na miradi mingine itakayobuniwa siku za usoni. Pia hii ni fursa kwa yeyote atakayeamua kufanya biashara kutumia umeme ili kujipatia kipato kama vile viwanda, wajasiliama (wachomeleaji, saluni na TEHAMA). Ndio faida ya kujenga miradi kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Mradi huu ni kielelezo cha mahusiano mazuri tuliyonayo kati ya Serikali zetu za Misri na Tanzania yaliyoanzishwa na viongozi wetu, Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Abdel Fattah Al-Sisi.

## **HITIMISHO**

Mwisho, nihitimishe kwa kuwashukuru wote mliofika katika hafla hii na wote mnaoendelea na utekelezaji wa mradi huu mkubwa na wa kihistoria kwa nchi yetu na mtambue kuwa matumaini makubwa ya watanzania yamebebwa na mradi huu. Hivyo, kazi zifanyike usiku na mchana bila kuchoka na kwa weledi mkubwa ili mradi ukamilike kwa ubora unaotakiwa na kwa wakati uliopangwa.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA!**